MASOMO YA SEKONDARI KUANZIA ALASIRI

(JUMAMOSI KUANZIA ASUBUHI)

Ni kwa wale watakaofanya mtihani wa maarifa (maarufu kama Q.T.) na mitihani mingine ya taifa kama watahiniwa wa kujitegemea.
Ebu, bweni la wavulana halina nafasi kwa ajili yao. Pole!

A. KWA WASIOWAHI KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE

Masomo yao yataanza
tarehe 10-1-2017.
Ada ni Tsh. 280,000 kwa mwaka.
Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 500,000, jumla ni Tsh 780,000.
Pamoja na masomo yaliyoorodheshwa hapa chini, wanaohitaji kufundishwa kwa nadharia na vitendo Physics, Chemistry na Information and Computer Studies watafanyiwa mpango nje ya ratiba kwa makubaliano maalumu
(nyongeza ya ada).

P I: KUJIANDAA MIAKA MIWILI KWA MTIHANI WA MAARIFA (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics).

I-II: KUJIANDAA MWAKA MMOJA KWA MTIHANI WA MAARIFA (Civics, History, Geography, English na Kiswahili).

P II: KUJIANDAA MWAKA MMOJA TENA KWA MTIHANI WA MAARIFA (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana na ile ya kidato cha kwanza.

P III: KUJIANDAA MIAKA MIWILI TENA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics;
au Civics, History, Geography, English, Literature na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana na ile ya kidato cha pili.

III-IV: KUJIANDAA MWAKA MMOJA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (Civics, History, Geography, English na Kiswahili).
Wanaotaka kujiunga wawe wamefaulu mtihani wa maarifa.

P IV: KUJIANDAA MWAKA MMOJA TENA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics;
au Civics, History, Geography, English, Literature na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana na ile ya kidato cha tatu na wawe wamefaulu mtihani wa maarifa.

Tunasisitiza kwamba masomo hayo si kwa watu wa kurisiti mtihani wa kidato cha nne. Kwa waliokwishafanya mtihani huo tumejipanga kuwaandaa kurisiti kwa miaka miwili au kwa mwaka mmoja tu kadiri ya hali yao upande wa elimu. Tazama mbele.

B. KWA WALIOKWISHAFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (HATA KAMA WAMEFELI)

Masomo yao yataanza
tarehe 10-1-2017.
Ada ni Tsh. 280,000 kwa mwaka.
Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 500,000. Jumla ni Tsh 780,000.
Pamoja na masomo yaliyoorodheshwa hapa chini, wanaohitaji kufundishwa kwa nadharia na vitendo Physics, Chemistry na Information and Computer Studies watafanyiwa mpango nje ya ratiba kwa makubaliano maalumu.

T I na T II (= TARATIBU MWAKA WA KWANZA NA TARATIBU MWAKA WA PILI): KUJIANDAA MIAKA MIWILI KURISITI MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics;
au Civics, History, Geography, English, Literature na Kiswahili).

H (= HARAKA): KUJIANDAA MWAKA MMOJA KURISITI MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (Civics, History, Geography, English na Kiswahili).

C. KUJIANDAA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA

V-VI: KUJIANDAA MWAKA MZIMA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (History, Kiswahili na Language; au History, Geography na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe wamepata credits (A, B au C) walau tatu katika masomo yoyote walipofanya au waliporisiti mtihani wa kidato cha nne. Wawe pia wamepata walau D katika somo la English.
Masomo yao yataanza tarehe 23-5-2017.
Ada ni Tsh. 480,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 580,000. Jumla ni Tsh 1,060,000.

KARIBUNI !

MASOMO YA SEKONDARI KUANZIA ASUBUHI

Ni elimu rasmi kwa wale tu wenye sifa za kufanya mitihani ya taifa kama wanafunzi wa shule; kwa wengine tuna masomo ya jioni (tazama nyuma).

F I: KUINGIA KIDATO CHA KWANZA
(Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics).
Wanaotaka kujiunga wawe wamezaliwa si kabla ya mwaka 2000 na kufaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2015 au 2016.
Usaili utafanyika tarehe 12-11-2016 na 17-12-2016 saa 2:00 asubuhi.
Washindi watatangazwa baada ya siku tatu na kuanza masomo tarehe 3 -1-2017.
Ada yao ni Tsh. 400,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wataongeza Tsh. 500,000. Jumla ni Tsh. 900,000.

F V: KUINGIA KIDATO CHA TANO
(History, Kiswahili na Language;
au History, Geography na Kiswahili;
au History, Geography na Language;
au Chemistry, Biology na Geography;
au Physics, Chemistry na Biology).
Wanaotaka kujiunga wawe: wamezaliwa si kabla ya mwaka 1995; wamefaulu (A, B, C au D) English;
wamepata credits (A, B au C) katika masomo yote waliyoyachagua walipofanya au waliporisiti mtihani wa kidato cha nne;
wamepata credit ya tatu mwaka 2015 au 2016.
Usaili utategemea vyeti tu (vya kuzaliwa au kumaliza shule na hati za matokeo ya kidato cha nne).
Washindi watatangazwa tarehe 12-6-2017 na kuanza masomo tarehe 4-7-2017.
Ada ni Tsh. 500,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wataongeza Tsh. 500,000. Jumla ni Tsh 1,000,000.

MAELEZO MUHIMU KWA WOTE

Shule yetu ni ya mchepuo wa sayansi.

Pamoja na masomo yaliyoorodheshwa, lile la Information and Computer Studies linafundishwa kwa nadharia na vitendo.

Wakristo wa madhehebu yote wanatakiwa kusoma pia Bible Knowledge au Divinity; kwa wengine ni hiari.

Ili kukwepa utapeli na ulanguzi, fomu za kujiunga zinapatikana hapa tu kwa Tsh. 20,000 na zinaweza kununuliwa hata siku ya usaili, mradi mhusika alete picha yake ya hivi karibuni au vielelezo vyote vinavyotakiwa.

Inawezekana pia kupakua fomu kutoka tovuti ya shule halafu kulipa shuleni Tsh. 20,000 kwa kuigonga mhuri unaoihalalisha. Usikubali fomu bila mhuri wetu.

Mbali na fomu, malipo yoyote yanatolewa risiti katika ofisi ya mhasibu; nje ya hapo malipo si halali, na shule haihusiki nayo, hata kama aliyepewa pesa ni mwalimu wetu. Jihadhari sana.

Ada zote za bweni na zile za masomo ya asubuhi zinaweza kulipwa kwa mikupuo minne, lakini zile za masomo ya mchana zinatakiwa kulipwa kwa mkupuo mmoja; zaidi ya ada hakuna mchango unaodaiwa na shule.

Taaluma inadai idadi ya wanafunzi darasani isizidi kiwango fulani, kumbe msongo wa wanaotaka kusoma kwetu ni mkubwa mno: ndiyo sababu ni lazima tuwachuje sana. Kudai kupokelewa nje ya taratibu zilizopangwa ni kuwadhuru kielimu waliokwishakubaliwa.

HATUNA NAFASI ZA KUHAMIA KIDATO CHA PILI, CHA TATU, CHA NNE WALA CHA SITA KUTOKA SHULE NYINGINE

JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO
ALFAGEMS SECONDARY SCHOOL (S.3874)
S.L.P. 6083 – MOROGORO
Tel. 0732-931605 (Ofisi)
0789-978886 (Airtel Money)
0752-452444 (kuwasiliana M-Pesa)
237405 (uwakala wetu M-Pesa)
0714-176745 (Bweni la kiume)
www.alfagems.com

Shule yetu inazingatia taaluma na maadili kwa kufuata sera ya elimu ya Kanisa Katoliki.

NAFASI ZA MASOMO

Tunawashukuru nyinyi, wananchi wote, kwa kuonyesha mmeipenda sana.

Pamoja na kuwaahidia juhudi endelevu za kuboresha huduma, tunawatangazia nafasi zifuatazo.

Tafadhali, kabla hamjanunua fomu za kujiunga, ulizeni vizuri kuhusu masomo yanayowafaa zaidi.

Baadaye hamtaruhusiwa kubadili fomu wala masomo, kwa sababu ni lazima twende kwa mpango.

Pre-form I: Wanaohitaji kujiandaa miezi mitatu ili kujiunga na kidato cha kwanza mwakani katika shule yoyote, masomo yatatolewa kuanzia tarehe 13 -9-2016 katika vituo vifuatavyo:
*Kigurunyembe Secondary School (katikati ya mji wa Morogoro)
*Malati Secondary School (mtaa wa Bigwa)
*Savannah Girls Centre (Mzumbe)
Ada ni Tsh. 90,000. Wanaohitaji kukaa bweni (wavulana Malati - wasichana Savannah) waongeze Tsh. 160,000. Jumla ni Tsh. 250,000.